



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA



TAARIFA KWA UMMA

KUKANUSHA TAARIFA ZA UPOTOSHAJI ZINAZOSAMBAA KUHUSU USAJILI WA WATOTO KUPITIA MPANGO WA *TOTO AFYA KADI*

Februari 5, 2024

1. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) unawatahadharisha wananchi wote kuhusu kuwepo kwa taarifa za upotoshaji zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu utaratibu wa usajili wa watoto kupitia mpango wa TOTO AFYA KADI na kudai gharama za usajili kuwa Sh. 35,780/= kwa mwaka na 95,780/= kwa miaka mitano na kutaka taarifa za mtoto zitumwe kwenye namba ya Whatsapp +255 735 051419.
2. **Taarifa hizo ni za upotoshaji na wananchi wanatahadharishwa kuzipuuza.** NHIF haifanyi usajili na kupokea nyaraka za wanachama kupitia Whatsapp wala kupokea michango ya wanachama kupitia namba za simu. Aidha viwango vya uchangiaji vilivyoonishwa ni vya upotoshaji.
3. Mfuko unaendelea kuwakumbusha wananchi kwamba unaendelea kusajili watoto kwa utaratibu zifuatazo:-
 - i. **kujiunga na mzazi/wazazi wao kupitia Vifurushi vya bima ya afya** ambapo michango hutegemea uchaguzi wa kifurushi husika na idadi ya wanaojiunga au
 - ii. **kupitia usajili wa ujumla wa wanafunzi kupitia shule wanazosoma** ambapo wazazi/walezi na uongozi wa shule husika huwasiliana na ofisi ya NHIF iliyo karibu kukamilisha usajili huo ambapo **kila mtoto atachangiwa Sh. 50,400 kwa mwaka.**
4. Michango ya wanachama **hulipwa kupitia namba ya malipo ya Serikali (control number)** inayotolewa na Mfuko baada ya kukamilisha usajili na si vinginevyo.
5. Wananchi wanakumbushwa kwamba mawasiliano na NHIF yanafanywa kwa kutumia mfumo rasmi wa mawasiliano uliowekwa na Mfuko ikiwemo namba ya **huduma kwa wateja 199, tovuti ya Mfuko ambayo ni www.nhif.or.tz** na akaunti za mitandao ya kijamii ya **Twitter, Instagram na Facebook kupitia @NHIFTZ.** Hivyo, mwananchi ahakiki taarifa ya NHIF kupitia njia hizo kabla ya kuchukua hatua kuitekeleza.

Imetolewa na;

Anjela Mziray

MENEJA UHUSIANO